

UGONJWA SIO KIFO

Mambo Gani Ufanye Unapogundua Unatatizo la Kiafya

MS. NATHALIA AYUB NKYA

© NATHALIA AYUB NKYA

Simu: 0718 664 741

Email: nadonjob1@gmail.com

Facebook: Natalie Nkya

Instagram: Natalie Nkya

Toleo la Kwanza 2024

Haki zote zimehifadhiwa!

Hairuhusiwi kutoa nakala sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa namna yoyote bila idhini ya mmiliki wa kitabu hiki, isipokuwa kwa kunukuu kuliko ruhusiwa kisheria.

Cover Design na Typesetting imefanywa vizuri na:

Lamax Designs, +255 764 793 105

lamaxdesigns@gmail.com

[\(Nawe Leta Kitabu chako tukupangie vizuri\)](#)

Kimehaririwa na; Prisca Charles | 0754393255

TABARUKU

Kwenu wanangu wapenzi *Jaleesa* na *Janeen*, ninyi ni ahadi na baraka ya Mungu iliyodhahiri. Mlizaliwa wakati mwanana, ujio wenu uliniletea kitabu hiki na kimebadilisha afya na maisha yangu kwa kiwango hali cha juu mno. Ninawaomba muwe watu bora, wenye thamani kwa vizazi vyenu hapo baadae.

Nawapenda sana.

SHUKRANI

Napenda kumshukuru Mungu kwa neema, wema na uaminifu wake katika maisha yangu hasa kwa kuniwezesha kuanza na hatimaye kumaliza uandishi wa kitabu hiki. Alinipigania na kuniponya afya yangu, hasa nyakati zote nilipokuwa katika maumivu makali, hali ya kukata tamaa lakini bado alikuwa pamoja nami na kuniimarisha.

Pia napenda kuishukuru familia yangu kwa maombi, malezi, usimamizi na kadhalika, daima nakumbuka namna mlivyopoteza vingi ili nisisimame tena na kurudi kwenye afya yangu ya awali, asanteni kwa nyakati zote ambazo mliacha vyote ili mnitunze mimi maana nilihitaji upendo na uangalizi wa hali ya juu. Mungu awabariki sana.

Vilevile bila kuwasahau marafiki na watu wangu wote wa karibu, ninawashukuru mno kwa namna mlivyosimama nami daima bila kuchoka kwa maombi, ushauri na kunitembelea toka enzi zile mpaka niliposimama imara.

Mwisho, napenda kukushukuru kaka yangu muiinjilisti *Charles Mushi* kwa kukubali kuwa mjumbe mwema wa siri za Mungu hasa pale alipokupa maneno ya kuniambia juu ya uandishi wa kitabu hiki, ninaamini kitabu hiki kitafanya yale Mungu aliyokusudia kwa watu wake sawa sawa na mapenzi yake.

DIBAJI

Kuta za hospitali zimesikia sala na dua nyingi za dhati kuliko kuta za makanisa, hekaluni, misikitini na nyumba zozote za ibada kwa ujumla. Wakati wa ugonjwa ni wakati nafsi ya mwanadamu inasononeka na kupata makunyanzi. Ugonjwa ni kipimo cha ukumbusho kwa mwanadamu kwamba haudumu milele. Pia wakati wa ugonjwa miili yetu hupata changamoto kwa kuchakaa na kuporomoka katika ubora wake. *“MWANADAMU ALIYEZALIWA NA MWANAMKE, SIKU ZAKE ZA KUISHI SI NYINGI. NAYE HUIJAA TAABU. YEYE HUCHANUA KAMA VILE UA, KISHA HUNYAUKA” - Ayubu 14: 1-2.*

Ugonjwa unapoingia swali la kwanza huwa ni JE, UNA TIBA? Hatamu ya kuendelea kutumaini huja kutokana na majibu ya swali hilo. Kitabu hiki cha **UGONJWA SI KIFO** ni kitabu kinachotoa uangavu wa majibu ya maswali haya yaani tumaini la kuendelea, namna ya kuacha hofu na kuanza kuishi. Haijalishi ni kwa kiasi gani lakini uponyaji wa kwanza huanza katika nafsi. Nafsi yenye nguvu ni kirutubisho cha uhai wa mwili. Chemchemi za tumaini na tanzu za matarajio ya kesho hujichechemua kutoka katika vilindi vya nafsi zetu.

Pia kitabu hiki ni sawa na uroto wa mifupa ambao uchochea uzalishwaji wa seli za mwili. Uroto uendao

kunyunyiza ndani ya nafsi na kukupa tumaini la kunyanyuka na kuuona uangavu wa kesho iliyo njema. Ni matumaini yangu nuru ilio ndani ya jumbe za kitabu hiki itaangazia nafsi yako.

“UGONJWA SI KIFO *ni tumaini la nyakati za giza zito kipindi cha udhaifu wa kimwili na kiroho. Ukabarikiwe na kuinuliwa. Naam ukahuishwe sawasawa na vipawa vya Mwenyezi Mungu. Amen!”* **Dr. Joshua. Lameck. Sultan PT**

UTANGULIZI

Kila mtu anapenda kuwa mwenye furaha, imara, mwenye nguvu bila kuwa na magonjwa, changamoto au maumivu ili afurahieuwepo wake duniani huku akiendelea kuishi na kuzitimiza ndoto zake. Ni ngumu kufanya chochote pale afya inapokuwa na tatizo yaani afya ya akili naafya ya hisia. Vitu hivi vinapoingia dosari, mfumo mzima wa maisha huathirika, lakini bado havipaswi kuwa ndio sababu ya kukuzuia wewe kuwa bora na kuishi vile ambavyo Mungu amekukusudia uwe au unavyotamani kibinafsi.

Kila mmoja wetu anatarajia pale anapokwenda hospitali kwa ajili ya vipimo au kumuona Daktari juu ya kupata maelezo au ufafanuzi wa kitabibu kwa yale maumivu anayoyapitia ili apatiwe msaada na kuweza kuwa sawa. Mara nyingi huwa tunatoka tukiwa tumepunguziwa au kutuliwa mzigo wa hofu na mashaka tuliyonayo ila mara nyingine huwa tunaondoka tukiwa na majibu yasiyofurahisha au nyongeza ya maumivu kutokana na majibu hayo na wengine huambulia kuambiwa hawajakutwa na tatizo lolote ilihali wanapata dalili zote za ugonjwa. Hali hii inaumiza hata kwa walio na tegemeo lao kwa Mungu, wanajiuliza kuwa kama yeye ni mponyaji, kwa nini ameruhusu mapito hayo badala ya kuwaponya. Kitabu hiki kimelenga kuwafungua macho na kuwatia

moyowale wote wanaopitia kwenye changamoto za afya hata kufikia hatua ya kuambiwa kwamba hakuna suluhu yeyote kulingana na changamoto wanayokumbana nayo, wanachongoja ni kifo tu.

Tutajifunza kwamba inawezekana kuendelea kuyaboresha na hata kubadilisha maisha yako maadamu upo hai. Kitabu hiki kimelenga kukuonesha kwamba inawezekana kutimiza ndoto ulizonazo, kuishi kwa furaha hata kama umebakiwa na mwezi mmoja tu wa kuishi. Pia kimelenga kukutoa kwenye shimo la hofuya kifo, aibu na kukufanya uwe jasiri na mpiganaji kwa ajili ya afya na kesho yako, uwe tayari kujifunza kwa kupitia shuhuda za watu wengine waliopambana na kuchomoka na kuyashinda yote yaletayo unyonge. Ugonjwa sio kifo unaweza kuishi kwa furaha na kutimiza ndoto zako.

Vilevile hata kwa wasio wagonjwa, kitabu hiki kinatoa fursa ya kujifunza kwa kuwa hakuna anayejua hatma ya afya yake kwa maana wapo waliokumbwa na changamoto katika kipindi fulani cha maisha ilihali walizaliwa bila ugumu wowote, pia kimelenga kukuonyesha kwamba maisha yana changamoto nyingi lakini nafasi ipo ya kunyanyuka na kuwa bora bila kutetereka pale utakapoamua binafsi.

JIPATIE HIKI KITABU LEO
(NUNUA) UWEZE KUELEWA
KWA UNDANI ZAIDI JUU YA
“UGONJWA SIO KIFO” NA
Mambo Gani Ufanye
Unapogundua Unatatizo la Kiafya

Piga Simu: 0718 664 741

Email: nadonjob1@gmail.com

KITABU KINA SURA TISA (9)